## Huduma zinazotolewa kwa manusura wa ukatili wa kijinsia

Huduma zifuatazo zinatolewa kwa watu wanaopitia ukatili wa kijinsia Tanzania. Huduma hizi zinatolewa na watoa/vituo vya kutolea msaada wa kisheria; polisi; afisa ustawi wa jamii; na vituo vya kutolea huduma za afya.

**Manusura wa ukatili wa kijinsia**

**Vituo vya kutolea msaada wa kisheria**

Kutoa mwongozo wa huduma zilizopo kwa manusura na wanapoweze kupata msaada; kutoa ushauri wa kisheria kwa manusura kuhusu haki zao na hatua za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa; na kufuatilia kesi zao.

**Polisi**

Kutoa fomu ya PF3; kupokea malalamiko; kukusanya ushahidi unaohusiana na kesi za ukatili wa kijinsia; na kuandaa faili la kesi dhidi ya mtuhumiwa wa kosa la ukatili wa kijinsia.

**Afisa ustawi wa jamii**

Kufanya mahojiano na kuwasaidia manusura; kuwasindikiza watoto waliopitia ukatili katika huduma zote zinazotolewa; Kutoa rufaa kupata huduma za kiafya, kisaikolojia na au Polisi; na kutengeneza na kutekeleza mpango wa matunzo na ulinzi unaozingatia mahitaji ya manusura.

**Vituo vya Afya**

Kutoa huduma za afya kama vile dawa kinga dhidi ya VVU na magonjwa ya ngono, dawa za kuzuia mimba, kutibu majeraha; ukusanyaji na uhifadhi wa vielelezo vinavyoashiria ukatili; kujaza fomu ya PF3 za manusura.

## Mambo muhimu ya kuzingatia kama umepitia ukatili wa kijinsia

- Kutoa taarifa ya matukio yote ya ukatili wa kijinsia katika Kituo cha Polisi.
- Epuka kubadilisha mavazi, kuoga, au kujisafisha mpaka baada ya Hospitali/Polisi ili usiharibu ushahidi.
- Hudhuria kituo cha kutolea huduma za afya ndani ya masaa 72 baada ya tukio la kubakwa au kulawitiwa ili kupata huduma za kinga dhidi ya VVU, magonjwa ya ngono na dawa za kuzuia mimba.
- Tafuta msaada kwa kuongea na mtu unayemuamini.

**Jamii isikae kimya kuzungumzia na kufichua vitendo vya ukatili wa kijinsia ili kudhibiti vitendo hivyo.**


**Mawasiliano**

Mradi wa 'Access to Justice for Women and Children / Society in Action for Equality' (SAFE),
Ofisi ya GIZ Tanzania, Nyumba Na. 76, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam, Tanzania
safeproject@giz.de


# Ukatili wa kijinsia

Elimisha • Pinga • Tokomeza

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

german cooperation DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

## Ukatili wa Kijinsia ni nini?

**Ukatili wa kijinsia ni kitendo kinachoelekezwa kwa mtu au kikundi cha watu kutokana na jinsi au jinsia zao au ukatili unaoathiri watu wa jinsia fulani. Hii ni pamoja na matendo yenye madhara ya kimwili, kingono, kihisia au yanayosababisha mateso kwa mtu.**

## Mifano ya Ukatili wa Kijinsia

### Ukatili wa Kimwili

Hii ni pamoja na ukeketaji, kumpiga, kumvua nguo, kumng'ata, kumchoma, kumtingisha, kumjeruhi, kumvuta nywele, kumtesa, kumkaba, kumkata, kumsababishia ulemavu au kumwua mtu. Kwa maneno mengine, ni kitendo cha kudhamiria kufanya vurugu na kutumia nguvu ili kumsababishia mtu madhara ya kimwili au mateso ambayo kwa asili sio ya kingono.

### Ukatili wa Kingono

Hiki ni kitendo cha kumlazimisha mtu kushiriki shughuli zozote za kingono bila kuridhia, ikiwa ni pamoja na vitendo vya kumwingilia au kutomwingilia kimwili na mara nyingine hata visivyo vya moja kwa moja. Matendo haya ni pamoja na ubakaji, ulawiti, kubusu, kushikwa mwili, kutongoza bila ridhaa, utakaso wa mjane, na mengineyo.

### Ukatili wa Kisaikolojia



Hiki ni kitendo anachofanyiwa mtu kwa lengo la kumsababishia madhara ya kiakili, kimawazo au kihisia. Ni matendo ya kudhalilisha au ya kushusha thamani, kuitwa majina mabaya, matendo ya kuaibisha au unyanyapaa au kutengwa, kupewa vitisho vya ukatili wa kimwili, pamoja na lugha ya matusi au maneno ya kufedhehesha.

### Ukatili wa Kiuchumi

Ukatili huu unamnyima mtu fursa za maendeleo na unahusisha ubaguzi katika fursa za kiuchumi. Hii inahusisha kunyimwa elimu, kutopewa haki ya kujihusisha kwenye shughuli za maendeleo, kumiliki mali, na kurithi mali, kutojihusisha katika majadiliano yanayohusu maendeleo, na unyanganyi wa mali miongoni mwa wajane.

### Ukatili Unaowezeshwa na Teknolojia

Hii inahusisha vitendo vya uvujishaji wa picha za faragha, kuvujisha taarifa za binafsi, unyanyasaji wa mitandaoni, pamoja na usambazaji wa picha za mtu za kubuni zinazokaribiana na uhalisia. Pia inajumuisha usambazaji wa chuki dhidi ya wanawake ikiwa ni pamoja na majaribio ya kuwanyamazisha au kuwashusha thamani wanawake mtandaoni. Mara nyingi huambatana na vitisho vya ukatili wa kimwili nje ya mtandao.

**Ukatili wa kijinsia unasababishwa na masuala mbalimbali ikiwemo:**

1. Uelewa mdogo kuhusu Sheria na haki za binadamu.
2. Tamaduni na mila potofu zilizopitwa na wakati kama vile ukeketaji, ndoa za utotoni, utakaso wa wajane, vipigo kwa wanawake kama adhabu.
3. Mfumo dume.
4. Kutokutoa taarifa dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na wakati mwingine kushirikiana na wanaotenda ukatili.
5. Kutopatikana kwa haki miongoni mwa manusura wa ukatili wa kijinsia kwa matukio ambayo yameripotiwa.
6. Matumizi ya pombe na madawa ya kulevya. Mfano: wanaume wanapotumia vilevi au madawa ya kulevya ni rahisi kutenda matukio ya ukatili wa kijinsia. Wanawake wanapotumia vilevi au madawa ya kulevya wanaweza kupelekea kutendewa matendo ya ukatili wa kijinsia.

## Madhara yanayosababishwa na ukatili wa kijinsia

Ukatili wa kijinsia unasababisha madhara mbalimbali ikiwemo; ukosefu wa amani, msongo wa mawazo, kukata tamaa na kutokujithamini, kuporomoka kwa maadili, mimba zisizotarajiwa, mimba katika umri mdogo, kuvunjika kwa familia au ndoa, kuongezeka kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kuambukizwa magonjwa ya ngono kama vile VVU, Kaswende, au Gono, na kupoteza maisha.